PACEMAKER SERIES - 005

DARASA LA TANO
JARIBIO LA MTIHANI
KISWAHILI - LUGHA

2015

JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU
1. Tumia penseli ya kawaida tu.
2. Hakikisha umeandika kwa karatasi ya majibu:-
i) JINA LAKO *(ii) JINA LA SHULE YAKO*

Muda: Saa 1 Dakika 40

Soma kifungu kifuatacho . Kina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo . Chagua jibu lifaalo kujazia nafasi

Wanafunzi wa shule ya Bidii ___1___ wakielezewa jinsi ya ___2___ maji. Kwa miaka ___3___ eneo ___4___ la shule hiyo lilikuwa limekauka kama ___5___ . Waliombwa kuhakikisha kuwa hawatumii maji___6___ . Eneo la Bidii lingebadilika iwapo maji___7___ .___8___ mvua ___9___ masika ___10___ walitakiwa kuchimba mabwawa ili___11___ maji ya mvua. Mwishowe wangetumia maji ___12___ kunyunyizia mashamba___13___ na kuvuna mazao___14___ na kupata vyakula___15___.

1.	A. ilikuwa	B. walikuwa	C. alikuwa	D. amekuwa
2.	A. kuhifadhi	B. kumwaga	C. kula	D. kupika
3.	A. nne	B. tatu	C. tano	D. sita
4.	A. zote	B. yote	C. lote	D. wote
5.	A. jangwa	B. maji	C. ugali	D. miti
6.	A. vizuri	B. ovyo	C. ipasavyo	D. vipasavyo
7.	A. ingepatikana	B. wangepatikana	C. yangepatikana	D. ilipatikana
8.	A. Hivyo basi	B. Kwao sasa	C. Hata hivyo	D. Kumbe
9.	A. wa	B. la	C. cha	D. ya
10.	A. uliponyesha	B. liliponyesha	C. kiliponyesha	D. iliponyesha
11.	A. kuutega	B. kuyatega	C. kulitega	D. kuitega
12.	A. hayo	B. hilo	C. hizo	D. huo
13.	A. zao	B. lao	C. wao	D yao
14.	A. nyingi	B. nyingine	C. mengi	D. wengi
15.	A nyingi	B. zingi	C. vingi	D. kingi

Kuanzia swali nambari 16 - 30, chagua jibu lifaalo.

16. Ndizi ambazo zimeiva huwa na rangi gani?

A. Manjano B. Nyeupe

C. Nyeusi D. Kijani

17. **Andika sentensi ifuatayo kwa wingi:**

Kitabu cha kuandikia huitwa daftari.

A. Vitabu za kuandikia huitwa daftari

B. Vitabu vya kuandikia huitwa daftari.

C. Vitabu vya kuandikia huitwa madaftari

D. Vitabu za kuandikia huitwa madaftari

18. **Kanusha:** Ninaenda sokoni kununua embe.

A. Siendi sokoni kununua embe.

B. Sijaenda sokoni kununua embe.

C. Sitaenda sokoni kununua embe

D. Sikuenda sokoni kununua embe

19. Maana ya semi: **aga dunia** ni

A. kufa B. kula

C. kuimba D. kutoroka

20. **Kamilisha methali ifuatayo:**

Haba na haba___

A. ni haba mbili B. hujaza kibaba

C. huleta kubaba D. hubabaisha sana

21. Chagua kundi ambalo linafanana

A. Kalamu, rula, gari, mtoto

B. Noti, meza, rula, sikio

C. Kibuyu, kiroboto, kikombe, kipepeo

D. Chai, soda, uji, maji

22. **Tegua kitendawili:**

Nimetoka ikulu nikiwa nimejishika kiuno

A. sikio B. kikombe

C. pikipiki D. ndege

23. Sakafu _____ itapigwa deki.

A. yote B. zote

C. wote D. nyote

24. Chagua sentensi iliyo katika wakati timilifu

A. Waliondoka asubuni na mapema.

B. Ameenda jikoni kula chakula

C. Wote wataadhibiwa kwa utovu wa nidhamu.

D. Wanafagia chumba cha kulala

25. Wanafunzi watano waligawana chungwa moja na kila mmoja akapata kipande sawa na wengine. Je kila mmoja alipata __

A. thumni B. humusi

C. sudusi D. subui

26. Tambua umbo lifuatalo



A. kipenyo B. mstari wima

C. mstari sambamba D. nusu kipenyo

27. Chagua sentensi sahihi

A. Kitabu yake imepotea

B. Kalamu lao limeanguka.

C. Taifa la Kenya lina watu wengi.

D. Miguu yao yanauma sana.

28. **Andika kinyume cha:** Hama

A. hamwa B. hamishwa

C. hamia D. hamisha

29. Wewe _____ uliyepita mtihani vizuri.

A. ndiwe B. ndiye

C. ndio D ndie

30. **Kamilisha sentensi**

Tamu kama

A. unga B. mandazi

C. uji D. asali

Soma ufahamu kisha ujibu maswali yafuatayo kuanzia 31 - 40

Hapo zamani za kale palikuwa na fisi. Fisi pia huitwa shumndwa. Alifanya urafiki na mwana wa mfalme. Kila walipopata nafasi walitembeleana. Mtoto wa mfalme alimjulisha baba yake kuhusu mgeni wake. Mfalme naye alimkaribisha kwa **mikono miwili** . Fisi naye alishukuru sana kwa kupata mwaliko huo.

Kuanzia hapo, fisi akawa mgeni wa mara kwa mara wa mfalme. Hapo aliweza kuvutiwa na binti ya mfalme . Aliomba posa na ikakubaliwa. Fisi alishukuru sana. Aliona ndoto yake ya kuwa na mke ilikuwa imetimia.

Walipokuwa wakiondoka kutoka bomani pa mfalme fisi aliwaona kondoo wanono karibu na lango. Alianza **kuwamezea mate.** Aliaapa kurudi wakati wa usiku na kumla mmoja. Kumbe hakuwa akitania. Usiku mkuu, alichechemea hadi walipokuwa kondoo. Alimla mmoja lakini alisikika. Alishikwa akiiba na akapigwa sana na famalia ya mfalme. Mfalme kuona hivyo, alibadilisha uamuzi wake wa awali. Aliamua kuwa binti yake hangeolewa na fisi mwenye tamaa.

31. Kukaribisha kwa mikono miwili huonyesha kuwa
    A. kuna huzuni
    B. kuna msiba
    C. kuna furaha
    D. kuna mabishano
32. Fisi alifanya urafiki na nani?
    A. Mwana wa punda
    B. Mwana wa mfalme
    C. Mwana wa rais
    D. Mwana wa kondoo
33. Fisi alitaka kumwoa
    A. malkia wa mfalme
    B. bibi ya mfalme
    C. binti ya mfalme
    D. kondoo wa mfalme
34. Fisi alitamani sana
    A. kuwa na bwana
    B. kuwa na ndoto
    C kuwa na mke
    D kuwa na mwana wa mfalme
35. Kondoo wa mfalme
    A. walikuwa wanono
    B walikuwa wakondefu
    C. walikuwa wajinga
    D. walikuwa washenzi
36. Kondoo wa mfalme walikuwa
    A. karibu na lango
    B. karibu na nyumba
    C. ndani ya nyumba
    D. nyuma ya lango
37. Kumezea mate ni sawa na
    A. kutoka mate
    B. kuangalia kwa makini
    C. kutamani
    D. kuhisi njaa
38. Kondoo waliibwa saa ngapi?
    A. Adhuhuri
    B. Asubuhi na mapema
    C. Usiku mchanga
    D. Usiku mkuu
39. Hali ya fisi kushikwa akimwiba kondoo inaelezwa na methali
    A. Asiyesikia la muu huvunjika guu
    B. Baada ya dhiki faraja
    C. Siku za mwizi ni arubaine
    D. Chururu si ndondondo
40. Mfalme alitaka binti yake aolewe na mtu
    A. asiye na tamaa
    B. mfalme kama yeye
    C. aliye na tamaa
    D. aliye na chuki

Soma kifungu kisha ujibu maswali 41 - 50

Hali ya hewa imebadilika sana. Joto limepanda sana na kuwa jingi zaidi.Hili ni jambo ambalo limewafanya wanasayansi kutoka kote ulimwenguni kuungana ili kutafuta suluhu ya tatizo hili. Mvua inanyesha bila kutarajiwa hasa hapa mjini Nairobi. Juzi nyumba zote zilikuwa zimezama . Nilishangaa nilipoona nyumba ya familia ya rafiki yangu Ouma ikiwa imejaa maji. Mvua hii haikutarajiwa na yeyote.

Baraza la jiji linastahili kuwa na mipango ya ni vipi linaweza kuzuia shida ya mafuriko. Mji wa Nairobi ulipata hasara kubwa sana , Barabara ziliharibika , nyumba zikabomoka na hasara kubwa zaidi ilikuwa vifo vya wakazi kumi na watatu.

Watabiri wa hali ya hewa nao lazima wajue kutoa utabiri wa kweli . Siku hizi watu wengi wanakosa imani nao. Swali ni je, kama watashindwa na majukumu yao, Mkenya wa kawaida atategemea nani?

41. Hali ya hewa imebadilika vipi ?
    A. Joto limepungua sana
    B. Joto limeongezeka sana
    C. Joto linapuliza sana
    D. Hakuna joto hata kidogo
42. Mvua inayonyesha mjini
    A. huwa haijatarajiwa
    B. huwa imetarajiwa
    C. ni ile ndogo ndogo
    D. haileti hasara hata kidogo
43. Nyumba iliyozama katika maji ni
    A. ile ya familia ya mwandishi
    B. ile ya familia ya rafiki ya mwandishi
    C. ile ya jamaa ya akina mwandishi
    D. ile ya jirani yake mwandishi
44. Mipango inastahili kutolewa na
    A. bodi ya jiji B. paneli ya jiji
    C. umati wa jiji D. baraza la jiji
45. Hasara kubwa kuliko zote iliyotokea jijini ilikuwa gani ?
    A. Barabara za lami kuharibika
    B. Nyumba kubomoka
    C. Maji kujaa katika nyumba
    D. Kuangamia kwa watu
46. Watabiri wa hali ya hewa
    A. huishi mbinguni
    B. ni sawa na Mungu
    C. wameokoka wote
    D. hueleza watu jinsi hali ya anga ilivyo
47. Dawa ya joto kuzidi inatafutwa na
    A. Wakenya wote
    B. wanasayansi wa Kenya
    C. wanasayansi wa dunia yote
    D. wanasayansi wa mbinguni
48. Jukumu la watabiri ni
    A. kutoa utabiri wa uongo
    B. kutoa utabiri wa kando
    C.kutoa utabiri wa kweli
    D. kutoa utabiri mrefu
49. Rafiki ya mwandishi aliitwa
    A. Onyango B. Ouma
    C. Umaa D. Mauma
50. Kichwa mwafaka kwa makala haya ni
    A. Mji wa Nairobi
    B. Joto jingi mjini
    C. Mvua ya masika
    D. Hali ya hewa mjini.